**JIMBO LA VERMONT**

**MAHAKAMA KUU** | **IDARA YA JINAI**
**Kitengo** | **Nambari ya Kesi**____________________

**Jimbo la Vermont dhidi ya**______________________ **Tarehe ya Kuzaliwa:**______________________

Anwani ya Mshtakiwa: ________________________________________________________

# MSAMAHA WA KUENDELEA KUFIKA MAHAKAMANI NA OMBI LA KUJIBU MASHTAKA

Mimi, ambaye ndiye Mshtakiwa aliyetajwa hapo juu, nimeshtakiwa kwa kosa/makosa ya_____________________________________, ambalo/ambayo ni makosa madogo chini ya sheria za Jimbo la Vermont. Ninaelewa kwamba adhabu ya juu zaidi ninayoweza kupokea kwa ajili ya kosa/makosa haya ni_________________________________.

Ninaelewa kwamba adhabu ya lazima ya kiwango cha chini zaidi ni:
☐ ____________________________________
☐ Haihusiki

(ikiwa shtaka limerekebishwa)
Nimepokea nakala ya Taarifa Zilizorekebishwa, ikiwa ni pamoja na adhabu ndogo zaidi na kubwa zaidi zinazoweza kutolewa kwa shtaka/mashtaka yaliyo katika hati hii. Ninajiondolea haki ya kusikilizwa kwa kesi ambapo nitasomewa mashtaka pamoja na adhabu, pamoja na haki zingine zinazohusiana na kusikilizwa kwa kesi hiyo.

Ninaelewa kwamba Mahakama inaweza kuamrisha kwamba mwathiriwa alipwe gharama ya hasara, kama ipo.

Ninaelewa kwamba ili kuthibitisha shtaka ninalokabiliwa nalo, sharti Jimbo lithibitishe vipengele muhimu vifuatavyo kwa viwango vinavyohitajika kisheria:

____________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________

Ninaelewa kwamba nina haki ya kuwakilishwa na wakili ambaye nitamgharamia mwenyewe, na kama siwezi kumudu huduma za wakili, ninaweza kupata wakili atakayeteuliwa na kugharamiwa na Jimbo.

☐ Siwakilishwi na wakili na sitaki kuwakilishwa na wakili.

☐ Ninawakilishwa na wakili, ambaye jina lake ni____________________________. Ninaridhishwa na ushauri na uwakilishaji ninaopata kutoka kwa wakili wangu.

Ninaelewa kwamba nikiwa mshtakiwa katika kesi ya jinai, nina haki za kikatiba na kisheria. Ninaelewa kwamba ninaweza kuendelea KUKANA MAKOSA ya shtaka lililopo hapo juu, na kwamba Jimbo lina jukumu la kuthibitisha kwamba nina makosa kwa kiwango kinachohitajika kisheria. Ninaelewa kwamba kwa KUKIRI KOSA au KUKUBALI ADHABU PASI NA KUKIRI KOSA, ninajiondolea haki zifuatazo, na kwamba Mahakama inaweza kunipa adhabu sawa na katika hali ambapo ningeendelea KUKANA KOSA, kesi yangu isikilizwe, kisha nihukumiwe na baraza la mahakama:

a. haki ya kusikilizwa kwa kesi yangu na baraza la mahakama;
b. haki ya kuhoji mashahidi wowote watakaotoa ushahidi dhidi yangu;
c. haki ya kuwasilisha ushahidi na kuletwa kwa mashahidi Mahakamani kwa ajili yangu kwa gharama ya Jimbo;
d. haki ya kukaa kimya kuhusiana na kosa ambalo nimeshtakiwa nalo;
e. haki ya kukata rufaa.

Hakuna vitisho au matumizi ya nguvu yoyote dhidi yangu yaliyofanywa na mtu yeyote ili kujaribu kunishurutisha kukiri kosa au nikubali adhabu pasi na kukiri kosa. Nakiri kosa au nakubali adhabu pasi na kukiri kosa kwa hiari yangu, kwa uhuru na kwa kujitoa mimi mwenyewe. Hakuna ahadi zozote nilizopewa na mtu yeyote au Jimbo, mbali na zile ambazo ziko katika Taarifa ya Mkataba wa Kujibu Mashtaka ulioambatishwa. Nakubali kwamba uamuzi wangu wa kukiri kosa umefanywa kwa msingi wa kweli, kuungwa mkono na hati ya kiapo inayoeleza kwamba kuna uwezekano kwamba nilitenda kosa hilo, na nakubali kwamba yafuatayo ni kweli:

____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________

Ninaelewa kwamba kwa KUKIRI KOSA, nakubali kwamba nilitenda sehemu kuu za kosa ambalo nimeshtakiwa kwalo. Ninaelewa kwamba kwa KUKUBALI ADHABU PASI NA KUKIRI KOSA, sikatai kwamba nilitenda sehemu kuu za shtaka/mashtaka hayo. Aidha, ninaelewa kwamba kwa KUKIRI KOSA au KUKUBALI ADHABU PASI NA KUKIRI KOSA la ukiukaji wa Kifungu cha 23 cha Maelezo ya Sheria za Vermont kunaweza **kusababisha kusitishwa kwa leseni yangu au haki ya kuendesha gari katika Jimbo la Vermont.** Ninaelewa kwamba KUKIRI KOSA au KUKUBALI ADHABU PASI NA KUKIRI KOSA kunaweza kuwa na adhabu zingine za ziada. Nimepitia Taarifa ya Adhabu za Ziada Zinazoweza Kutokana na Hukumu zilizo kwenye upande wa nyuma wa mkataba wa kukiri shtaka ulioambatishwa. **Aidha, ninaelewa kwamba, kama mimi sio raia wa nchi ya Marekani, KUKIRI KOSA au KUKUBALI ADHABU PASI NA KUKIRI KOSA kunaweza kunisababishia adhabu ya kufukuzwa nchini, kunyimwa uraia wa Marekani, au kutokubaliwa kuingia tena nchini Marekani.**

Hivyo, naiomba Mahakama ikubali ☐ KUKIRI KOSA ☐ KUKUBALI ADHABU PASI NA KUKIRI KOSA kwa shtaka/mashtaka yaliyoorodheshwa hapo juu.
Kwa kuwasilisha ombi hili, najiondolea haki zangu za kisheria kwa mujibu wa sheria ya V.R.Cr.P. 32 na sitaki kutoa maelezo kwa niaba yangu au kutoa taarifa zozote zinazohusiana na hukumu au wakili wangu kuzungumza kwa niaba yangu. Hakukuwa na ripoti ya uchunguzi wa awali kabla ya kutolewa hukumu yangu, katika kesi yangu.

☐ Naiomba Mahakama ikubali kukiri kwangu shtaka/mashtaka yaliyoorodheshwa hapo juu na initoze kiasi cha $___________kama faini na ada ya ziada, na nakubali kulipa kiasi hiki. Ninaelewa kwamba ikiwa sitalipa kiasi hiki chote, salio lolote litakalobaki litadaiwa na wakala ya ukusanyaji madeni. Nimeambatisha hundi au hawala ya fedha yenye kiasi cha $______________ itakayolipwa kwa Mahakama Kuu ya Vermont kwa ajili ya malipo ya faini iliyotozwa na Mahakama, pamoja na ada za ziada za lazima za Mahakama zinazotumika

☐ Ninaiomba Mahakama ikubali kukiri kwangu shtaka/mashtaka yaliyoorodheshwa hapo juu na itoe Hati ya Kufungwa Gerezani ya kifungo cha kati ya siku _________________ hadi ________________ ili kutumikia kifungo kinachoniruhusu kwenda kazini mchana na kurudi gerezani usiku kupitia mpango ulioidhinishwa awali. Ninaelewa kwamba kushindwa kumaliza kutumikia kifungo hiki kinachoniruhusu kwenda kazini mchana na kurudi gerezani usiku kupitia mpango ulioidhinishwa awali kunaweza kusababisha nitumikie muda utakaobaki kwenye kifungo changu nikiwa gerezani. Ninaelewa kwamba Mahakama pia itatoza ada ya ziada ya lazima kwa kila shtaka ambalo NIMEKIRI KOSA au NIMEKUBALI ADHABU PASI NA KUKIRI KOSA. Ninakubali kuripoti katika Idara ya Uangalizi wa Wahalifu si zaidi ya saa___________ ☐ asubuhi ☐ adhuhuri/alasiri mnamo_________________ ili kuratibu wakati wa kutolewa kwa hukumu hii.

☐ Ninaiomba Mahakama ikubali kukiri kwangu shtaka/mashtaka yaliyoorodheshwa hapo juu na kutoa Amri ya Kuweka Mhalifu Chini ya Idara ya Uangalizi inayotoa hukumu iliyo katika Notisi ya Mkataba wa Kujibu Mashtaka ulioambatishwa pamoja na Amri ya Kuweka Mhalifu Chini ya Idara ya Uangalizi iliyoambatishwa. Nimepitia masharti yote ya kawaida na maalum yanayotumika ya kipindi cha uangalizi, na kwa kutia saini yangu hati hiyo, ninakubali masharti hayo yanayotumika. Ninaelewa kwamba Mahakama itanitoza ada ya ziada ya lazima kwa kila shtaka ambalo nimejibu kwa KUKIRI KOSA au KUKUBALI ADHABU PASI NA KUKIRI KOSA. Ninaelewa kwamba, wakati wa kipindi changu cha uangalizi, ikiwa sitafuata masharti ya kawaida na maalum yanayotumika, Mahakama inaweza kunipa adhabu isiyozidi ile inayolingana na mashtaka haya ambayo imeandikwa kwenye Taarifa ya Mkataba wa Kujibu Mashtaka iliyoambatishwa pamoja na Amri ya Kuweka Mhalifu Chini ya Idara ya Uangalizi iliyoambatishwa.

Ninakubali kuripoti kwenye Idara ya Uangalizi wa Wahalifu kufikia si zaidi ya saa__________ ☐ asubuhi ☐ adhuhuri/alasiri mnamo_________________ ili kukutana na Afisa wangu wa Uangalizi wa Wahalifu.

☐ Ninaomba Mahakama ikubali kukiri kwangu shtaka/mashtaka yaliyo hapo juu na iahirishe kutoa hukumu kwa kipindi cha miezi/miaka _________________ na itoe Amri ya Kuahirisha Hukumu Huku Mhalifu Akiwa Chini ya Uangalizi yenye masharti yaliyoandikwa kwenye Taarifa ya Mkataba wa Kujibu Mashtaka iliyoambatishwa pamoja na Amri ya Kuahirisha Hukumu Huku Mhalifu Akiwa Chini ya Uangalizi iliyoambatishwa. Nimepitia masharti yote ya kawaida na maalum ya uangalizi wa wahalifu yanayotumika, na kwa kutia saini kwenye hati hiyo, ninakubali masharti hayo yanayotumika. Ninakubali kwamba katika wakati ambao kutolewa kwa hukumu yangu kutaahirishwa huku nikiwa chini ya usimamizi wa idara ya uangalizi wa wahalifu, ikiwa sitafuata masharti ya mkataba huu, Mahakama inaweza kunipa adhabu isiyozidi ya juu zaidi iliyoandikwa hapo juu pamoja na adhabu na ada zozote za ziada za lazima za kiwango cha chini zaidi zinazotumika. Ninakubali kuripoti kwenye Idara ya Uangalizi wa Wahalifu si zaidi ya saa__________ ☐ asubuhi ☐ adhuhuri/alasiri mnamo_________________ ili kukutana na Afisa wangu wa Uangalizi wa Wahalifu.

Ninaiomba Mahakama ikubali kukiri kwangu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa sababu kuhitaji kwamba nifike Mahakamani kunaweza kunitatiza kwa njia ifuatayo:

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**Tarehe**

_________________________________ _________________________________

**Saini ya Mshtakiwa**

_________________________________ _________________________________

**Saini ya Mlezi Kisheria**
*(ikiwa mshtakiwa ana umri chini ya miaka 18)*

**Saini ya Wakili wa Mshtakiwa**

Jimbo linakubali ombi la Msamaha wa Kutofika Mahakamani na, kwa mujibu wa Sura ya 5321 ya Kifungu cha 13 cha Maelezo ya Sheria za Vermont, Jimbo la Vermont lina maoni kwamba:

☐ hakuna mwathiriwa.

☐ mwathariwa/waathiriwa wamepewa taarifa ya awali ya kubadilika kwa jibu la mashtaka la mshtakiwa pamoja na haki yake ya kufika Mahakamani ili kutoa maoni yake kwa njia bayana kuhusu kosa la jinai lililotendeka, mtu aliyehukumiwa, na haja ya kurejeshewa gharama za hasara. Mwathiriwa/waathiriwa hawapo na hawajaeleza, kwa mdomo au maandishi, maoni yake/yao kuhusu kutolewa kwa hukumu au hoja inayopendekezwa ya kuahirishwa kwa utolewaji wa hukumu.

**Tarehe**

_________________________________ _________________________________

**Saini ya Wakili wa Jimbo**

**AMRI**

☐ Ninatambua kwamba kufika Mahakamani kwa mshtakiwa kunaweza kusababisha ugumu kuliko manufaa yoyote, na ninakubali jibu la mshtakiwa la mashtaka yaliyoorodheshwa hapo juu, huku nikifahamu kwamba amefanya uamuzi huo kwa hiari yake na akifahamu na kuelewa matokeo ya uamuzi huo baada ya kufahamu kuwa anajiondolea haki za kikatiba. Kukiri shtaka/mashtaka kumefanywa kwa msingi wa taarifa za kweli. Nimefikia uamuzi kwamba mshtakiwa ana makosa na kutoa hukumu ya kumkuta mshtakiwa na makosa.

☐ Sikubali ombi la mshtakiwa la kupokea msamaha wa kutofika Mahakamani kwa ajili ya shtaka/mashtaka yaliyoorodheshwa hapo juu.

**Tarehe**

_________________________________ _________________________________

**Saini ya Jaji**